# KUFUNGA
## Reloaded



Shemeji Melayeki

# KUFUNGA Reloaded!

**Shemeji Melayeki**

**Kufunga Reloaded! ©2019 Shemeji Melayeki**

**Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.**

SIMU: +255 714 548 565/+255 763 965 297

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
YouTube: *Shemeji Melayeki*
Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*
Twitter: *@melayeki*
Facebook: *Ap Shemeji Melayeki*

**ISBN 978-9976-5427-9-0**

Kimepigwa chapa na: ***CLIMAX SOLUTIONS - ARUSHA***

**+255 658 288 054**

**+255 687 699 862**

**+255 763 965 297**

**Jalada la nje limetengenezwa na DL BOOKSTORE SANAWARI- ARUSHA**

# YALIYOMO


**UTANGULIZI** ........................................................................ iii

**KUFUNGA AU KUSHINDA NJAA?** ................................. 1

**NIFUNGE SIKU NGAPI?** .................................................. 5

**HATARI YA KUFUNGA**................................................... 7

**KUFUNGA KINAFIKI** ....................................................... 9

**MALENGO MAKUU YA KUFUNGA NINI?**................. 14

**KUFUNGA NI ZAIDI YA KUACHA KULA**.................. 19

**MUHIMU** .......................................................................... 27

**UTANGULIZI**

Kufunga ni jambo muhimu sana kwenye maisha ya kila mwamini. Kwenye baadhi ya nchi swala la kufunga limekuwa hata la kisiasa…actually hii siyo kufunga bali ni mgomo wa kula “hunger strikes”.

Suala la kufunga halikuanza jana, Musa, Daudi, Eliya, wafalme wa Israel, manabii kama Daniel, Ezra, Nehemia, Esta, Hana, Yohana, viongozi na mitume wa kanisa la mwanzo, Paulo na hata Kornelio. Cha ajabu zaidi Bwana wetu Yesu Kristo, ALIFUNGA.

Kuna wakristo wana miaka hata 10 tangu waokoke hawajawahi kufunga, na hata wengine hawajui umuhimu wa kufunga. Au pengine hawakuwahi hata kufundishwa juu ya kufunga.

Kuna wakati mtu anaweza akafunga kwa siri yeye peke yake au ukafanya mfungo wa watu wote/jamii fulani ya watu USISHANGAE MTU AKIENDESHA MFUNGO WA KITAIFA AUJUMUIYA YA KIKANISA, KAMPUNI n.k.

Ukifuatilia kwenye biblia, kufunga kumetumika namna zifutazo:-

*Nēsteuō* ikiwa na maana ya kuacha kula KIGIRIKI (Agano jipya) au*tsûm* ikiwa na maana ya kufunga mdomo KIEBRANIA (Agano la Kale)

Katika maana mbili, unagundua kuwa kufunga ni kuacha kula (siyo kuacha kunywa) mbele ya tafsiri ya Kiebrania wameongezea neno *religiously* huku mwandishi akionyesha kuwa siyo mgomo wa kula wa kisiasa bali kwa ajili ya maswala ya *kidini/kiroho*….

KUFUNGA NI JAMBO LA UAMUZI KABISA KUACHA KULA KWA SABABU MAALUMU…

# KUFUNGA AU KUSHINDA NJAA?

Ukisoma Matendo ya Mitume 23:12-13 kuna watu waliapa kutokula hadi watakapomuua Paulo, jambo ambalo pia siyo mfungo… Je, waliacha kula? Ndiyo. Je, hii sababu ilikuwa maalum? Ndiyo. *Kulipopambauka, Wayahudi wakafanya mapatano, wakajifunga kwa kiapo kwamba hawatakula wala hawatakunywa hata wamwue Paulo. Na hao walioapiana hivyo walipata zaidi ya watu arobaini*. HATUONI SEHEMU YOYOTE KIAPO CHAO KIKITIMIA..

Kwa hiyo sababu ya mtu kufunga iwe ya kiroho na yenye kuzaa matunda katika ufalme wa Mungu.

Kufunga si kuacha kula ili kupunguza uzito au kutengeneza "shape" La, hasha. Ijapokuwa *lengo hilo pia si baya…*

Kufunga si kwa sababu umekosa chakula kwa hiyo unajitangazia *"Ohh sasa bora nifunge tu hakuna namna"*

Mwili ni kwa chakula. Kufunga ni kuunyima mwili chakula na hii ina athari nzuri zaidi kwa roho ya mtu.

Kufunga haingalii matokeo katika mwili bali katika roho na faida zitakazotokea kwenye ulimwengu wa roho. Mtu anapofunga kuna jambo analobadili/kutengeneza katika ulimwengu wa roho hasa pale ambapo hatua zilizozoeleka zitashindwa au zimeshindwa.

IJAPOKUWA KUNA FAIDA ZA KIMWILI ZA KUFUNGA KAMA KUPUNGUA UZITO, LAKINI SIYO SHABAHA YAKE….

MAMBO MUHIMU YANAYOAMBATANA NA KUFUNGA NI….*Kusoma na kutafakari neno, kuomba kwa bidii.*

Mtu aliyefunga kwa sababu za kiroho mara nyingi roho yake inatamani kula kuliko hata mwili wake hivyo hutamani zaidi chakula cha roho kuliko cha mwili yaani *neno na maombi.*

Yesu alipomaliza kufunga alihisi njaa ila siyo kiu. Hii inaonyesha kuwa kufunga ni lazima kuacha kula na siyo lazima kuacha kunywa maji.

Mathayo 4:2 *Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa.*

Kuna umuhimu mkubwa wa kunywa maji hasa unapokuwa kwenye mfungo wa siku zaidi ya tatu, wakati wengine wanaweza kufunga siku tatu bila kula wala kunywa lakini haishauriwi iwe zaidi ya siku tatu…

Musa alifunga siku 40 bila kula wala kunywa, nakuhakikishia kwa mazingira aliyokuwa nayo Musa

mbele za Bwana hata maji yangekuwepo asingeweza kuyanywa kwa sababu ya uzito ‘intensity’ ya uwepo wa Mungu. Mtu akiwa kwenye hali aliyokuwa nayo Musa hujikuta amefunga bila kupanga.

Esta anamwambia Modekai, Esta 4:16 *Uende ukawakusanye Wayahudi wote waliopo hapa Shushani, mkafunge kwa ajili yangu; msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana, nami na wajakazi wangu tutafunga vile vile; kisha nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria; nami nikiangamia, na niangamie.*

Paulo pia alifunga siku tatu, Matendo ya Mitume 9:9 *Akawa siku tatu haoni; hali, wala hanywi.*
Danieli alifunga wiki tatu au siku 21, angalia jinsi alivyofunga Danieli 10:2-3 *Katika siku zile mimi, Danieli, nalikuwa nikiomboleza muda wa majuma matatu kamili. Sikula chakula kitamu, wala nyama wala divai haikuingia kinywani mwangu, wala sikujipaka mafuta kabisa, hata majuma matatu kamili yalipotimia.*

Hakula chakula kitamu, wala nyama wala divai, wala kujipaka mafuta kabisa. Kwa lugha rahisi aliacha milo pendwa …kuna watu hawawezi kustahimili siku bila kunywa soda baridi… Upo? Au kula vitu fulani fulani amazing….kuna mtu kuacha kuingia facebook kwa wiki anaweza kujisikia kuumwa….asipoingia ni kama mtu

aliyesahau kupaka mafuta… anajisikiaje? Kuacha vitu vinavyopendwa yaweza kuwa sehemu ya mfungo pia.

**Unaona Aina Tatu Za Kufunga**

1. Kufunga kavu bila maji wala chakula
2. Kufunga isiyo kavu maji bila chakula
3. Kuacha nusu kuacha vyakula vitamu, nyama, vinywaji pamoja na mambo uliyozoea

**NIFUNGE SIKU NGAPI?**

Mtu mmoja aliwahi kuuliza nifunge lini? Nifunge siku ngapi?

Kwenye maandiko matakatifu kuna mifungo imeonyeshwa kuanzia nusu siku hadi siku 40 MFALME DARIO alifunga usiku tu.. na hakupata starehe ya kifalme akimwombea Danieli. Angalia Danieli 6:18 *Kisha mfalme akaenda nyumbani kwake, akakesha usiku kucha, akafunga; na vinanda havikuletwa mbele yake; na usingizi wake ukampaa.*
Inawezakana mfalme alikuwa analala siku zote kwenye *"amusement park"* yaani sehemu yenye muziki mlaini wenye uwezo wa kubembelezea usingizi mwororo.

Israeli walifunga siku moja Nehemia 9:1 *Hata siku ya ishirini na nne ya mwezi huo wana wa Israeli wakawa wamekusanyika, wakifunga, wenye kuvaa magunia, na kujitia udongo vichwani.*

Tumeona Paulo, Esta na Wayahudi walifunga siku tatu
Kornelio yeye alifunga siku nne,
Matendo ya Mitume 10:30

> *Kornelio akasema, Siku tatu zilizopita, katika saa ii hii, yaani saa tisa, nilikuwa nikisali nyumbani mwangu; nikamwona mtu amesimama mbele yangu, mwenye nguo zing'arazo.*

Wengine kama Daudi (2 Sam. 12:15-18) na wenyeji wa Yabesh-Gileadi 1 Samuel 31:11-13 walifunga siku saba

Paulo na watu aliokuwa nao walifunga siku kumi na nne Matendo ya Mitume 27:33 *Na kulipokuwa kukipambauka Paulo akawasihi wote wale chakula, akisema, Leo ni siku ya kumi na nne kungoja na kufunga, hamkula kitu cho chote.*

Tumeona pia kuwa Danieli alifunga siku 21 huku Musa, Eliya na Yesu wakifunga siku arobaini…

Kwa mtu ambaye hajawahi kufunga, ni vizuri kujifunza kufunga nusu siku (*kwa mfano saa kumi na mbili za mchana halafu anafungua jioni*) baadaye nusu mfungo kwa siku moja, mbili na kuendelea….

# HATARI YA KUFUNGA

Nimewahi kusikia mtu alifunga sana na baadaye akafariki, hata habari hizi zimekuwa nyingi kwa nchi za wenzetu kama India n.k. Ningependa kutoa tahadhari na mambo kadhaa ya kuangalia unapofunga. Hii itakusaidia uutunze mwili wako ambao ni hekalu la Mungu na kuepuka hasara za ujinga ambao adui anaweza kuutumia…

1… Ukiwa kwenye mfungo mrefu hakikisha unapata muda wa kutosha kulala,
2... Ni vizuri kuoga mara nyingi uwezavyo, kwani wengine huacha kabisa hata kuoga, hii pia huifanya mwili wako uendelee kufanya kazi vizuri.
3... Kama unatumia dawa za mara kwa mara mfano za TB, kisukari, n.k ni vyema kuongea na daktari wako hasa kama utapitisha mlo au zaidi. Hii ni kwa sababu unaweza kuwa unatumia vidonge au dawa inayohitaji ule aina Fulani ya vyakula au pengine dawa ambazo haziwezi kutumika bila kula vizuri. Hapa utapata ushauri wa kitaalamu.
4... Kusikia kuchoka, kuumwa kichwa au hata kizunguzungu zaweza kutokea hatua za mwanzo za mfungo. Hizi hupotea baada ya siku moja au mbili.
5... Njaa yaweza kukubana wakati wa mlo wa siku zote, ni vizuri kunywa maji wakati huo badala ya kuamua kula.

6… Kabla na baada ya mfungo inashauriwa kula vyakula vifaavyo (Nilisikia kuna mtu alitoka kwenye maombi ya siku 14 akaanza kula mahindi ya kuchoma na akafariki) hivyo pata vyakula kama uji, juices, matunda unapojiandaa. (ukitoka kwenye mfungo yafaa UNYWE KITU CHA MOTO kama uji au aina nyingine ya mlo kulingana na mazingira yako)..
7.. Siyo afya kutumia kahawa/chai wakati wa mfungo (hizi ni stimulants)
8… Usijitahidi kula na kushiba wakati wa kufungua ni vyema kula taratibu tena vyakula vilaini ili tumbo lako lirudi katika hali yake ya mwanzo. Kumbuka utumbo hujibana (shrinks) mtu anaokuwa amefunga muda mrefu. Kwa sababu ya ulaini 'delicacy' ya utumbo uwe taratibu unapoanza kula.
Kama hujazoea kujiongoza kwa ngazi hiyo omba hata mtu akusaidie wakati wa kufungu.

HII NI KWA FAIDA ZAIDI ITOKANAYO NA MFUNGO WAKO.
Usitumie kanuni za watu kwenye kufunga mbona fulani alifanya hivi MIILI YETU NI TOFAUTI… LEARN YOUR STYLE…

Watu wakiitisha mfungo ni vyema kuangalia ule ambao utauweza! Au omba ushauri unapoanza mfungo kwa mchungaji wako, mentor, au kiongozi wa kiroho.

# KUFUNGA KINAFIKI

Kufunga siyo jambo lililopitwa na wakati, kabla ya kuja kwa Yesu watu walikuwa wanafunga, hata wakati wa Yesu, aliwahi kuulizwa swali juu ya kufunga wala hakukataa habari za kufunga ila aliweka mkazo juu ya sababu na nia iliyoko ndani ya mfungaji.
Yesu alishughulikia zaidi nia ya mfungaji….

Mathayo 6:16-19

> *Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.*

HAPA, unaona Yesu akishughulikia wale wafungaji wanaofanya SHOW OFF kwenye kufunga. Kama unataka kujionyesha sawa, ukionekana si unakuwa umepata ulichokuwa umenia?

HAPO, YESU ALIKUWA ANAONGEA NA WANAFUNZI WAKE, HII NI KUSEMA…KILA ALIYE MWANAFUNZI WA YESU ANATAKIWA KUJUA KUFUNGA IPASAVYO…

Anaposema ***Bali wewe ufungapo***, ni dhahiri kuwa anategemea watu hawa kufunga…

WANAFUNZI WA YESU WALIKUWA HAWAFUNGI ILA YESU ALITOLEA MAELEZO KUWA HAWAHITAJI KUFUNGA WAKATI YUPO BADO NAO KATIKA HALI YA MWILI…

Marko 2:18-20

> *Nao wanafunzi wake Yohana na Mafarisayo walikuwa wakifunga; basi walikuja, wakamwambia, Kwani wanafunzi wa Yohana na wanafunzi wa Mafarisayo hufunga, bali wanafunzi wako hawafungi? Yesu akawaambia, Walioalikwa arusini wawezaje kufunga maadamu bwana-arusi yupo pamoja nao? Muda wote walipo na bwana-arusi pamoja nao hawawezi kufunga. Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana-arusi, ndipo watakapofunga siku ile.*

Hii ni dhahiri kwamba sisi ambao ni wanafunzi/disciples wa Yesu tunatakiwa kufunga katika nyakati zetu kwani YESU ALISEMA, lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana-arusi, ndipo watakapofunga siku ile. Kusema *watakapoondolewa bwana-arusi* maana yake ni kwamba *hawatahitaji kufunga akiwapo* lakini akiondoka watafunga. Je, kuna haja ya kumtafuta mtu wa kukujibu maswali yako wakati unajua mwalimu yupo karibu? La hasha. Utauliza maswali papo hapo.

Kwa hiyo hawakuwa na haja ya kufunga kwali walikuwa na mwenye majibu yao karibu nao, lakini akiondolewa ni sawa wakifunga.

Lengo la kufunga siyo kuonekana au kujionyesha kwa watu YESU ANASEMA Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.

Haimaanishi watu wakikuuliza kwa nini hauli chakula waambie nimefunga wala siyo uwaambie *"niko mlimani"* kama wengine wanavyofanya. Hata hivyo wengine hupata shida zaidi mpaka hata kudiriki *kudanganya*. Mpendwa, uatajitesa sana. Cha muhimu ni moyo wako lengo lako kama ni kuonekana hata pozi utakaloweka wakati wowote ni kutaka kuonekana. Wanafiki wakifunga nia yao ni kutaka kuonekana na watu. Yaani wakati wanaandaa mfungo tayari wanajua wanataka nini. KUONEKANA. Hivyo hujitahidi kutangaza (kutangaza siyo mbaya kama kuna haja ya watu kujua) kwa lengo la kujionyesha; pengine aonekane yuko rohoni sana au ni mtakatifu au mlokole kuliko wengine. Hayo ni malengo mabaya ya mfungo.

Haina haja ya kufunga na kuelekeza moyo wako kwa watu ambao hawawezi kukupa haja ya moyo wako ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.

Ndiyo maana Isaya anaeleza kwenye Isaya 58:3 *Husema, Mbona tumefunga, lakini huoni? Mbona tumejitaabisha nafsi zetu, lakini huangalii? Fahamuni, siku ya kufunga kwenu mnatafuta anasa zenu wenyewe, na kuwalemea wote watendao kazi kwenu.*

Watu wengine wakifunga wanaomba excuses kwenye kazi zote za nyumbani au ofisini kisa wamefunga HAYA NI MATANGAZO YANAYOASHIRIA KUTAKA KUONEKANA NA WATU KUWA UMEFUNGA... Ukifanya hivyo Mungu hana thawabu ya kukupa kwani waliokuona wanatosha…

HATA KAMA MNAFUNGA KAMA KIKUNDI SIYO UTANGAZE KILA SEHEMU KUWA NIMEFUNGA NA KIKUNDI CHANGU, WEWE TAFUTA KUONEKANA NA BABA (YAANI MPAJI WA MAHITAJI YAKO)

Mtu anayefunga anatafuta kuonekana AIDHA na watu AU na Baba aonaye sirini...

CHUNGUZA NIA YAKO WAKATI WA MFUNGO, ILI USIJE KUMUULIZA MUNGU  Mbona tumefunga, lakini huoni? Mbona tumejitaabisha nafsi zetu, lakini huangalii?

NB: Hatufungi ili kupambana na shetani bali kuonekana mbele za Baba Yetu aonaye sirini.. KUMLINGANA BWANA.

THE FOCUS IS NEITHER MEN NOR DEVIL BUT OUR PRECIOUS FATHER…

## MALENGO MAKUU YA KUFUNGA NINI?

Katika kuonekana mbele za Baba aonaye sirini kwa ajili ya mambo yetu, kuna ,mambo kadhaa maandiko yameweka wazi,
Zaburi 35:13b *Nalijitesa nafsi yangu kwa kufunga…* niliamua kufuatilia hili neno nalijitesa kwenye tafsiri nyingi za kingereza wametumia neno humbled.

Hili neno limetumika Kiebrania kama ʽ*ânâh* ikimaanisha kujitesa au kujinyenyekeza ili kuweza kuwa makini, kutazama kwa umakini (take heed or pay attention) KWA HIYO kufunga ni kuufanya mwili uipe roho ya mwanadamu kunasa au kusikia kitu kutoka kwa Mungu kwa urahisi zaidi. Inaonekana mwili ukiwa na nguvu sana inainyima roho ku download vitu kwa Roho wa Mungu.

Kwenye nafsi ndipo palipo na mawazo (akili), nia na hisia… Kufunga kunaifanya mawazo, nia na hisia zikubaliane au kuelewa na kutenda (katika mwili) lile ambalo ni sawa sawa kabisa na neno la Mungu au kusudi/shauri la Mungu. Mtu aliyeshiba mpaka anacheua anaweza zaidi kupotezea sauti ya Mungu kuliko mtu aliyefunga…

Usifunge tu kwa sababu watu wanafunga… ELEWA HIVI…. roho ya mwanadamu, huchukua vitu vya

Mungu kutoka kwa Roho wa Mungu (anayechunguza mambo ya ndani ya Mungu) na kuleta kwa nafsi ya mwanadamu… Nafsi, ikielewa sawa sawa huamuru mwili kutenda sawasawa..

KWA HIYO, KUFUNGA HUIFANYA ROHO YA MWANADAMU KUWA NA NGUVU JUU YA NAFSI NA MWILI KUYATII YALE AMBAYO BABA ALIYEKO SIRINI ANAYASEMA ILI KUYAFANYA…

Je, Hii si bora kabisa? Badala ya kupapasa papasa unajua ni nini mapenzi ya Baba katika yale unayoyapitia.

Wakati tunaendelea, hebu tafakari hili Zekaria 7:5 *Waambie watu wote wa nchi, na hao makuhani, ukisema, Hapo mlipofunga na kuomboleza katika mwezi wa tano na mwezi wa saba, katika miaka hiyo sabini, je! Mlinifungia mimi kwa lo lote; mlinifungia mimi?*

YESU ALIPOKUWA ANAKWENDA KUJARIBIWA WAKATI ANAELEKEA KWENYE MFUNGO…

Luka 4:1-2

> *Na Yesu, hali amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Yordani, akaongozwa na Roho muda wa siku arobaini nyikani, akijaribiwa na Ibilisi. Na siku hizo alikuwa hali kitu; hata zilipotimia, aliona njaa.*

ALIPORUDI KUTOKA KWENYE MFUNGO…

Luka 4:14

> *Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando.*

Yesu alirudi na nguvu (dunamis) baada ya kushinda majaribu aliyojaribiwa na Ibilisi, ukiangalia maneno aliyokuwa anasema Ibilisi siyo uongo ila siyo sauti ya Baba hata kama imeandikwa kama Baba hakusema haifai kufuata…

YESU ALISHINDA MAJARIBU MATATU AMBAYO HAWA (MKE WA ADAMU) ALISHINDWA

Mwanzo 3:6 *Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.*

1….Tamaa ya Mwili/tumbo> ule mti wafaa kwa chakula FOOD

2….Tamaa ya Macho> wapendeza macho EYES

3… Kiburi cha Uzima> mti wa kutamanika kwa maarifa WISE

Soma Luka 4:3-9

1….Tamaa ya Mwili/tumbo> iambie jiwe hili liwe mkate YESU ANGEONA INAFAA KWA CHAKULA
2….Tamaa ya Macho> akamwonyesha milki zote za ulimwengu ANGEPENDEZWA NA HILO PIA…
3… Kiburi cha Uzima> Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini PAMOJA NA UHAKIKA KWAMBA MALAIKA WATAAGIZWA HAKUFANYA HIVYO..

1 Yohana 2:16

> *Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia.*

HII NDIYO PRODUCTS KUU ZA IBILISI , tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, MUNGU HANA HIZO PRODUCTS..

Roho Mtakatifu kwa kusoma majira ya mambo yatakayomtokea mbele na akijua mwili na nafsi yake yaweza kuwa kikwazo cha majibu ya maombi yake, akamwongoza kwenye kufunga muda wa siku 40. Na hapo Yesu alishinda majaribu matatu aliyojaribiwa Hawa na Kushindwa kabisa...

Ndiyo maana mwanzoni nilisema mfungo unakuandaa kwa ajili ya hali inayokuja mbele yako ili uweze

kushinda kwa hekima ya Mungu na siyo ya mwanadamu..

MFUNGO... Unakusaidia kuwa na SPIRITUAL ATTENTION/KUWA MAKINI NA SAUTI YA MUNGU kuweka kuchuja sauti ya Mungu na ya adui na kukusaidia KUTII kwa urahisi kile cha Mungu bila kuingiliwa na sauti za nafsi wala matendo ya mwili..

MFUNGO UNAKUSAIDIA USIFUATE tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima BALI SAUTI YA BABA AONAYE SIRINI…

Watu wengi wamedanganywa kwamba wakifunga wanapata nguvu za kumshinda Ibilisi, ila hapana… INAKUSAIDIA KUTAMBUA TOFAUTI KATI YA HILA ZA IBILISI NA KWELI YA NENO LA MUNGU.

# KUFUNGA NI ZAIDI YA KUACHA KULA

Mwanzoni, nilitangulia kusema kuacha tu kula bila kufanya chochote kitakachohuisha roho yako ni mgomo wa kula/hunger strike

Kufunga ni zaidi ya kuacha kula… HEBU TAZAMA HAPA

Yeremia 36:6 *Basi, enenda wewe, ukasome katika gombo la chuo, ambacho umeandika ndani yake, maneno ya Bwana yaliyotoka kinywani mwangu, ukiyasoma katika masikio ya watu, ndani ya nyumba ya Bwana,* ***siku ya kufunga; pia utayasoma masikioni mwa watu wote wa Yuda, watokao katika miji yao.***

SIKU YA KUFUNGA KUNA KAZI ILIFANYIKA… Nehemia 9:1,3 *Hata siku ya ishirini na nne ya mwezi huo wana wa Israeli wakawa wamekusanyika, wakifunga, wenye kuvaa magunia, na kujitia udongo vichwani. Basi wakasimama mahali pao,* ***wakasoma katika kitabu cha torati ya Bwana, Mungu wao, muda wa robo ya siku; na robo nyingine wakaungama, wakamwabudu Bwana, Mungu wao.***

UMEONA KAZI NYINGINE?

**MAMBO MAKUU MAWILI YALIFANYIKA KUOMBA NA KUTAFUTA KUSIKIA KUTOKA KWA BWANA:**

(Ndiyo maana wakasoma NENO LA BWANA)

HIVYO KUFUNGA NA KUOMBA NA KUTAFAKARI NENO HAVIACHANI…

Kufunga siku 20 na kujikuta siku zote 20 unapuyanga tu kuzunguka mjini ni kupoteza milo yako..labda kama lengo lako ni kupunguza uzito. Watu wengi sana wanafunga na kutumia muda kuzunguka tu barabarani mjini halafu wanarudi jioni kufungua. Huu sio mfungo ni kupitisha tu muda wa kula. Hebu fikiria kijana wa dotcom anafunga na bado anakaa mtandaoni kuperuzi picha na kuchati Instagram, Facebook, Twitter n.k huku anaangalia saa kama muda wa kufungua umefika au la. Huu sio mfungo.

Nikiwa nafanya kazi benki kazi iliyokuwa imenishikilia sana... kila mara nikiwa kwenye mfungo nilikuwa Napata shida sana... kwani muda mwingine nilikuwa busy, nika-develop utaratibu mmoja… ulionisaidia, WAKATI break ya lunch nilikuwa najifungia sehemu na kuomba.. Sometimes store (stoo) sometimes hata washrooms (maliwato) kwa namna yoyote nisiwe nimepitisha mgomo wa kula... nikifika nyumbani

natafuta angalau nusu saa ya kujifungia na kuomba na wakati mwingine naomba zaidi ya saa moja.

Kusema ukweli kufunga ukiwa kwenye shughuli zako za kila siku hauna matokeo ukifananisha na mtu anayetumia muda wake kukaa katika utulivu akimtafakari Mungu na Neno lake. Hii ni tofauti ya kushinda njaa na kufunga.

**Hebu Angalia**

Matendo ya Mitume 13:3

> *Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao.*

Luka 2:37 …

> *ila huabudu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba.*

Matendo ya Mitume 14:23

> *Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga,*

Danieli 9:3

> *Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga..*

Nehemia 1:4

> *Hata ikawa niliposikia maneno hayo, nikaketi, nikalia, nikaomboleza siku kadha wa kadha; kisha nikafunga, nikaomba mbele za Mungu wa mbinguni.*

**Luka 5:33** …. *hufunga mara nyingi, na kuomba dua…*

Matendo ya Mitume 10:30

> *Kornelio akasema, Siku tatu zilizopita, katika saa ii hii, yaani saa tisa, nilikuwa nikisali nyumbani mwangu; nikamwona mtu amesimama mbele yangu, mwenye nguo zing'arazo,*

Uwe kama KORNELIO, hata kama bize kiasi gani, TAFUTA MUDA WA KUOMBA…
Fikiria kama Kornelio angefunga tu bila kwenda kuomba ilipofika saa tisa HUYO MALAIKA PENGINE ANGEENDELEA KUHADITHIWA…. Kufunga, kunaongeza USIKIVU WAKO na KUFUNGUA MACHO YA (ndani) ROHO YAKO kwa hiyo jizoeze kuomba kila mara unapofunga…

**Hakuna Faida Yoyote Kufunga Bila Kuomba…**
Ukisoma DANIELI 9 (SOMA YOTE), utagundua baada ya Danieli kuona kuna kitu hakiko sawa na muda unazidi kuyoyoma na hana strategy ya kuwatoa ndugu zake Babeli akaingia kwenye kufunga na kuomba….pamoja na mambo mengine mengi.

## ANGALIA HAWA NDUGU WALIOFUNGA

Baada ya kujifunza baadhi ya kanuni za msingi za kufunga, hebu tutazame baadhi ya watu waliofunga

katika Biblia na matokeo ya kufunga kwao, ili tuone kanuni zitakazotusaidia pia…

**Hana Alifunga Na Kuomba….**

Hana alikuwa na tatizo binafsi (hakuwa na mtoto), lakini wakati wa mfungo akabadili mtazamo wa maombi yake kutoka kuomba mtoto hadi kuomba mtumishi atakayetumika kwenye kipindi kigumu cha ukosefu wa mafunuo dhahiri

1 Samweli 1:7-11

> *Tena mumewe akafanya hivyo mwaka kwa mwaka, hapo yule mwanamke alipokwea kwenda nyumbani kwa Bwana, ndivyo yule (PENINA) alivyomchokoza; basi, kwa hiyo, yeye akalia, asile chakula. Elkana mumewe akamwambia, Hana, unalilia nini? Kwani huli chakula? Kwa nini moyo wako una huzuni? Je! Mimi si bora kwako kuliko watoto kumi? Ndipo Hana akainuka, walipokwisha kula na kunywa huko Shilo. Naye Eli, kuhani, alikuwa akiketi kitini pake penye mwimo wa hekalu la Bwana. Naye huyo mwanamke alikuwa na uchungu rohoni mwake, akamwomba Bwana akalia sana. Akaweka nadhiri, akasema, Ee Bwana wa majeshi, ikiwa wewe utaliangalia teso la mjakazi wako, na kunikumbuka, wala usinisahau mimi*

*mjakazi wako, na kunipa mimi mjakazi wako mtoto mume, ndipo mimi (nitakapompa Bwana huyo mtoto siku zote za maisha yake, wala wembe hautamfikilia kichwani kamwe.*

**Mambo Yafuatayo Nimeyaona**

Hana alipofunga, akabadili aina ya maombi kutoka kutaka mtoto hadi mtumishi.

Aliacha kuomba mtoto akatoa nadhiri.

Kufunga na kuomba kwake kulimfanya Mungu kumfungua tumbo.

Alipofunga alifunguliwa macho na kujua ya kuwa Mungu hakutaka tu mtoto kuzaliwa bali aina ya mtoto atakayezaliwa.

**Kufunga Kunakufanya Utafute Zaidi nia/Mapenzi Ya Mungu Kwenye Jambo Unaloliombea Zaidi Ya Mapenzi Yako Tu…**

NI SAWA NA KUSEMA… Mathayo 6:10 Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

KUYAOMBA MAPENZI YA MUNGU UKIWA UMEFUNGA NI RAHISI ZAIDI KULIKO UKIWA HUJAFUNGA…. (Kumbuka mwanzoni nilipozungumza juu ya MWILI NA MAPENZI YA MUNGU)

Warumi 8:8

*Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.*

**Nehemia Alifunga Na Kuomba**

Nehemia 1:2-5

*Hanani, mmoja wa ndugu zangu, akanijia, yeye na watu wengine waliotoka Yuda; nami nikawauliza habari za Wayahudi waliopona, hao watu wa uhamisho waliosalia; na habari za Yerusalemu. Wakaniambia, Watu wa uhamisho, waliosalia huko katika wilaya ile, wamo katika hali ya dhiki nyingi na mashutumu; tena ukuta wa Yerusalemu umebomolewa, na malango yake yameteketezwa kwa moto. Hata ikawa niliposikia maneno hayo, nikaketi, nikalia, nikaomboleza siku kadha wa kadha; kisha nikafunga, nikaomba mbele za Mungu wa mbinguni; nikasema, Nakusihi, Ee Bwana, Mungu wa mbinguni, Mungu mkuu, mwenye kuogofya, mwenye kutimiza agano lake na rehema zake kwa hao wampendao na kuzishika amri zake;*

**Esta Afunga Na Wayahudi**

Esta 4:15-17

> *Basi Esta akawatuma ili wamjibu Mordekai, Uende ukawakusanye Wayahudi wote waliopo hapa Shushani, mkafunge kwa ajili yangu; msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana, nami na wajakazi wangu tutafunga vile vile; kisha nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria; nami nikiangamia, na niangamie. Basi Mordekai akaenda zake, akafanya yote kama vile Esta alivyomwagiza.*

Sasa naamini umeona baadhi ya watu waliofunga wakiwa na sababu hasa ya kuona jambo fulani linabadilika katika maisha yao na maisha ya watu wengine.

## MUHIMU

Kufunga ni kumwelekea Mungu kwa moyo wako wote na kutaka kusikia kutoka kwake mapenzi yake yaliyo mazuri na makamilifu. Hii ni kwa sababu mafanikio yako yote yanategema sana kuishi katika mapenzi yake. Watu wengine hutumia muda huu muhimu wa kuongea na Baba yetu wa mbinguni kupambana na mapepo, kuvunja laana mbalimbali badala ya kuongea na Baba juu ya ahadi zake na juu ya mahitaji yako. Tumia muda wako mzuri wa kufunga kuongea na kumsikiliza Baba, narudia tena….. *kuongea na kumsikiliza Baba*.

# Vitabu vingine vya Shemeji Melayeki

1. *Principles for Greatness*
2. *Principles of Growth*
3. *The Power of Vision*
4. *The Power of Taking the First Step*
5. *The Power of Reading Books*
6. *Nguzo za Siku: Msingi wa Kwanza*
7. *Nguzo za Siku: Msingi wa Pili*
8. *Ukombozi Reloaded*
9. *Utajiri wa Ukoo*
10. *Siku 14 za Maajabu*

# KUFUNGA

*Reloaded*

Kati ya mambo nimekuwa nikiyafuatilia kwa makini ni swala la kufunga, mbali na kwamba ni jambo la muhimu lakini pia watu wengi hawajui kufunga ni nini, inafanyikaje, kwa watu gani, matokeo yake na kwa nini hasa tufunge. Kufanya jambo usilolielewa kwa sababu kila mtu anafanya itakunyima kupata matokeo unayostahili kuyapata. Kitabu hiki ni uwanja wa mafunzo kukupa mwanga juu ya suala la kufunga.



0763965297
0714548565
@melayeki
Shemeji Melayeki
Ap Shemeji Melayeki
apostle_shemeji_melayeki
shemeji.melayeki@gmail.com

*Shemeji Melayeki*

DL BOOKSTORE
ISBN 978-9976-5427-9-0